Department of Health

# Habari zaidi kuhusu ukeketaji wa wanawake (FGM)

More information about FGM (Swahili)

Ukeketaji Wa Wanawake ni utaratibu ambapo viungo vya siri vya wanawake hujeruhiwa au hubadilishwa, lakini hakuna sababu za kimatibabu katika tendo hili. Jambo hili linaweza kuathiri sana afya ya wanawake na watoto wa kike katika maisha yao ya baadae. Wasichana wengine hufariki kutokana na kupoteza damu au kwa ugonjwa wa kuambukizwa kutokana na utaratibu huu. Wanawake waliokeketwa wanaweza kupata matatizo wakati wa uzazi.

kwa kawaida ukeketwaji hufanywa kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 5 na 10. Kunaweza kujulikana kama kutahiriwa kwa wanawake, kukata au maneno mengine kama vile sunna, gudniin, halalays, tahur, megrez na khitan kiwa ni pamoja na menginewe.

## Aina za Kukeketa:

| | |
|---|---|
| Aina ya kwanza - | Kuondolewa kwa sehemu au jumla kwa kinembe / kisimi |
| Aina ya pili - | Kuondolewa kwa sehemu au jumla ya kisimi na midomo ya ndani ya uke (ni ile "midomo" inayozunguka uke) |
| Aina ya tatu - | Kutolewa kwa kupunguza au kukata kwa jumla kwa uke, ikiwa ni pamoja na kisimi. Kushonwa kwa mwisho wa midomo ya uke na kuacha tundu dogo. |
| Aina ya nne - | taratibu zingine zote zenye madhara ikiwa ni pamoja na kukata, kuchoma, kurarua, kutoboa na kutanua sehemu za siri za uke. |

## Kwa nini ukeketwaji hufanywa?

Kwa kawaida wazazi wa msichana au ndugu na jamaa zake hufanya mipango ili yeye akeketwe. Sababu za kukeketa ni pamoja na:

- desturi
- dini
- kuhifadhi utamaduni
- kuhifadhi bikira
- usafi
- kulinda heshima ya familia
- kukubalika katika jamii, haswa kuhusiana na ndoa

Sababu hizi za ukeketaji zimejengwa katika kutokuelewa au kutokuwa na ufahamu.

Wengine wanaamini kuwa ukeketaji hutakiwa kufanywa ikiwa ni sehemu ya dini yao, kwa mfano aina ya kwanza ya ukeketwaji huitwa sunna kimakosa. Lakini **hakuna** kitabu chochote cha dini kinachounga mkono ukeketwaji au kinachosema kuwa tendo hilo lifanywe.

## Ukeketwaji ni kinyume cha sheria

Ukeketwaji ni kinyume cha sheria na ni lazima **kamwe** usitendwe hapa au nje ya nchi. Pia ni kinyume cha sheria kumsaidia mtu yeyote kufanya ukeketwaji wa namna yoyote. Yeyote atakayepatikana na kosa la hatia ya kukeketa ataweza kufungwa kwa muda wa miaka isiyozidi 14 na ataweza kutozwa faini (yaani atalazimika kulipa faini kama adhabu)

## Kukeketa kunaleta madhara mabaya katika afya yako

Kukeketa kunaleta madhara mabaya kwa wasichana na wanawake ikiwa ni pamopja na:

- maumivu yasiyopungua
- magonjwa ya kuambukizwa ya mara kwa mara ambayo yanaweza kukufanya uwe tasa (usiweze kuzaa)
- kutoka damu, uvimbe na majipu
- matatizo wakati wa kukojoa au kuvuja
- mfadhaiko wa akili, kumbukumbu mbaya, kujiumiza
- matatizo ya uzazi ambayo huweza kuleta kifo

## Msaada gani unaweza kupata?

Kama uliwahi kukeketwa unaweza kupata msaada wa matibabu kutoka kwa daktari wako (GP) au kutoka kwa bingwa yeyote wa afya. Unaweza kupata msaada kutoka kwa mkunga wako kama wewe ni mjamzito.

Pia unaweza kupata habari zaidi kuhusu kliniki na huduma za wataalamu wa ukeketwaji hapo www.nhs.uk/fgm.

**Kama una wasiwasi kuhusu msichana yeyote ambaye yumo hatarini kuhusu kukeketwa, mwarifu mtaalamu wa afya anayekutibu wewe au piga simu ya kupata msaada ya NSPCC 0800 028 3550, masaa 24 kwa siku.**

**kama una wasiwasi kuwa utalazimishwa na familia yako au jamii yako ili mototo wako wa kike akeketwe, mwulize daktari wako, mhusika wa afya au mtaalamu yeyote wa afya ili akusaidie**

## Pasipoti ya Afya

Unaweza kuomba nakala za 'tamko dhidi ya ukeketaji wa wanawake'. Hichi ni kijarida kidogo cha tamko ambacho kimechapishwa, kinapatikana katika lugha 11 na unaweza kukichukua ukienda nje ya nchi. Unaweza kukionesha kwa familia yako. Kinafafanua wazi kwamba ukeketaji ni kosa la jinai Uingereza.

## Kukusanya na kutumia habari kutoka kwa wagonjwa wa Ukeketaji Wa Wanawake (FGM)

NHS Digital inakusanya habari kuhusu Ukeketaji wa wanawake ndani ya Uingereza kwa niaba ya Idara ya Afya na Huduma ya Afya(NHS) Uingereza. Ukusanyaji wa habari hii unaitwa FGM Enhanced Dataset- www.content.digital.nhs.uk/fgm. Habari inayokusanywa inatumika kutoa maelezo ambayo yanasaidia kuboresha jinsi NHS inahudumia wanawake na wasichana ambao wamepitia au wako katika hatari ya Ukeketaji.

NHS Digital inakusanya kiwango cha habari ambayo ni ya ‘siri za kibinafsi’ kukuhusu kama vile jina lako, tarehe ya kuzaliwa, namba yako ya NHS na nchi uliyozaliwa. Inakusanya pia habari maalum inayohusu Ukeketaji wa wanawake. Hii ni pamoja na aina ya Ukeketaji, umri wako wakati ukeketaji ulifanyika, nchi ambayo ukeketaji ulifanyika na historia ya familia kuhusu Ukeketaji.

Madakatari wa kibinafsi (GPs) na wahudumu wengine wa afya wanahitajika kisheria kuipatia habari hii NHS Digital, lakini unaweza kupinga habari yako ya kibinafsi kushirikishwa. Unaweza kuzungumza na mtaalamu wako wa afya jinsi ya kufanya hivi. Au kujua zaidi kuhusu ambavyo habari yako inatumika na kusimamiwa, ikiwa ni pamoja na jinsi NHS Digital inadumisha siri za habari hii na kusajili pingamizi zozote tafadhali nenda kwa:

www.content.digital.nhs.uk/patientconf

**Kama unataka habari zaidi kuhusu ukeketaji wa wanawake, tafadhali nenda kwa www.nhs.uk/fgm**

© Crown copyright 2016 (haki zote zimehifadhiwa)
2905947 - Swahili 11/16
Imetengenezwa na Williams Lea kwa niaba ya Idara ya Afya
www.dh.gov.uk/publications